**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**650** **HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3.** **Mwaka : 2013**

---

**MAELEKEZO.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**

2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka sehemu **B**.

3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** ina alama **sitini (60)**.

4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.

5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Wazazi katika shule fulani walilalamika kuwa michezo inawapotezea Watoto wao muda wa kusoma. Ukiwa mwalimu, eleza hoja nne zitakazothibitisha umuhimu wa michezo kwa wanafunzi.
2. Wakati wa maandalizi ya somo, baadhi ya walimu huandika malengo yasiyo wazi. Eleza sifa nne zinazotofautisha lengo mahsusi bora.
3. Afisa michezo wa wilaya amehoji kwa nini tathmini iendelee kufanywa mara kwa mara. Eleza hoja nne za kuthibitisha umuhimu wa tathmini ya mara kwa mara.
4. Baadhi ya walimu huona vitabu vya kiada pekee vinatosha kufundishia. Eleza hoja nne za kuonyesha umuhimu wa vitabu vya ziada.
5. Katika maandalizi ya michezo, mwalimu anatakiwa kuwa makini. Eleza mambo manne yanayothibitisha umuhimu wa maandalizi ya vifaa na zana.
6. Wakati wa michezo, mwalimu anaweza kubaini matatizo ya kiafya ya wanafunzi. Eleza viashiria vinne vinavyoonyesha mwanafunzi ana matatizo hayo.
7. Shule nyingi zina ukosefu wa vifaa vya michezo. Eleza stadi nne zinazohitajika ili mwalimu aweze kutengeneza zana bora kwa kutumia vifaa vilivyopo.
8. Usalama wa wanafunzi wakati wa michezo ni jukumu la mwalimu. Eleza mambo manne muhimu ya kuzingatia.
9. Uliombwa kuandaa Azimio la Kazi kwa muhula mpya. Eleza zana nne muhimu na matumizi yake.
10. Wizara ya Elimu ina mpango wa kukagua vitabu shuleni. Eleza vigezo vinne vya kuzingatia kabla ya kuidhinisha kitabu cha Haiba na Michezo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali manne katika sehemu hii.

11. "Mwalimu anaweza kufundisha kwa uzoefu bila muhtasari." Kwa hoja tano, kanusha kauli hii.

12. Eleza mambo matano yanayoweza kuathiri mwenendo wa tabia za wanafunzi kupitia michezo shuleni.

13. Ajali za michezo huleta hofu kwa wazazi. Eleza njia tano za kuhakikisha usalama wa wanafunzi wakati wa michezo.

14. Andalio la somo ni nyenzo muhimu ya kufanikisha somo. Eleza namna vipengele vitano vya andalio vinavyotumika.

15. Azimio la Kazi ni maandalizi ya lazima. Eleza vipengele vitano na nafasi yake katika maandalizi ya somo.

16. Ripoti ya maendeleo ya mwanafunzi ni kumbukumbu muhimu. Eleza hoja tano za kuthibitisha umuhimu wa ripoti hiyo katika ufundishaji.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org